**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Pili - Tarehe 13 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 10

**Kuboresha Huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali awamu tatu za uongozi zilifanikiwa kuboresha huduma za afya nchini kwa kiwango kikubwa; na kwa kuwa Serikali katika Awamu ya Nne ya uongozi imejidhatiti kuhimiza huduma bora zaidi za afya kwa kuendelea kuzipatia vifaa vya kisasa hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali; na kwa kuwa Wilaya ya Kahama yenye wakazi takriban 750,000 inayo hospitali moja ya Wilaya ambayo pia inahudumia Wilaya ya Bukombe na vituo vya afya zaidi ya vinne;

(a) Je, ni lini Serikali itaipatia Hospitali ya Wilaya ya Kahama mashine mpya ya *X-ray* kwani mashine iliyopo imeshindwa kukidhi mahitaji?

(b) Je, ni lini Serikali itavipatia magari ya wagonjwa vituo vya afya vya Bulungwa na Ulowa ambavyo vipo mbali na hospitali ya Wilaya na vipo kwenye maeneo yenye watu wengi?

(c) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imetimiza azma yake katika Wilaya ya Kahama ya kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka watoto 95 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Lembeli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilikwishaipatia Hospitali ya Wilaya ya Kahama mashine mpya kupitia mradi wa *ORET* wa kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa nchini. Aidha, kila Hospitali ya Wilaya ilipatiwa mashine ya *X-ray* na *Ultrasound*.

Wakati huo Wilaya ya Bukombe haikuwa na hospitali yake, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tayari imekwisha kuingiza hospitali mpya ya Wilaya ya Bukombe kwenye mradi wa *ORET* utakofadhiliwa kwa pamoja baina ya Serikali yetu na Uholanzi. Hospitali zote mpya za Wilaya zitanufaika na mradi huu pia. Kwa utaratibu huu hospitali ya Wilaya ya Kahama itapunguziwa mzigo wa huduma za *X-ray* kwa vile Bukombe nayo itakuwa na *X-ray* yake kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2008.

(b) Ununuzi wa gari la wagonjwa ni jukumu la Halmashauri. Hivyo napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kuwasiliana na Halmashauri yake ili kuhakikisha kuwa mipango ya ununuzi wa gari la wagonjwa kwa vituo vya afya Bulungwa na Ulowa inawekwa kwenye Bajeti.

(c) Kitaifa vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 99 mwaka 1999 hadi 68 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2000. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 40 kwa vizazi hai 1000 mwaka 1999 hadi 36 kwa vizazi hai 1000 kwa mwaka 2000. Serikali imeweka mikakati kadhaa ya kupunguza vifo hivi.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuendeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya watoto kwa uwiano *(Integrated Management of Childhood Illness (IMCI)* mkakati wa kuharakisha kupunguza vifo vya akinamama vinavyotokana na uzazi *(road map)*, mkakati wa *IMCI*, unatekelezwa katika Wilaya zote nchini, Kahama ikiwa mojawapo. Wilaya ya Kahama ilianza utekelezaji wa mkakati huu tangu mwaka 2004. Mkakati huu unahusisha kutoa mafunzo kwa watoa huduma na jamii. Vituo vya mafunzo ya afya ya Kanda vinaharakisha utekelezaji wa mkakati huu ili kuweza kuwafikia walengwa wote.

Ili kuharakisha kupunguza vifo vya watoto wachanga, Serikali imeshakamilisha mpango wa utekelezaji wa mkakati wa *road map*. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itaanza utekelezaji wa kupunguza vifo vya watoto wachanga (*essential new born care)*. Mategemeo yetu ni kwamba Wilaya husika zitaingiza mikakati hii katika mipango ya mwaka.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Hospitali hii ya Kahama ni moja ya Hospitali za siku nyingi sana hapa nchini na miundombinu yake yote kwa kiasi kikubwa imeharibika sana ikiwemo hasa miundombinu ya mifumo ya maji taka na wodi za wagonjwa hasa wodi ya wazazi ambao kwa kiasi kikubwa

imeshakuwa ni ndogo kutokana na ongezeko la wagonjwa; je, Serikali ina mpango gani wa ujumla wa kupanua miundombinu ya hospitali hii na kuiboresha iwe ya kisasa ili kuendana na idadi kubwa ya wagonjwa na kukua kwa *population* ya Kahama? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutengeneza miundombinu ambayo ni chakavu katika hospitali huwa ni jukumu la Halmashauri husika na kama hospitali ile ni ya zamani mimi ningeshauri basi iweze kuwekwa katika mipango yao mkakati ili kuweza kuona kwamba wanaweza kutengeneza. Lakini vile vile ningependa kumshauri kwamba ipo *basket fund* ambayo inatumika katika masuala ya ukarabati. Kwa hiyo, kama ni suala la ukarabati wanaweza wakatumia fedha hiyo watakavyoona inafaa ili kuweza kufanya matengenezo. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni azma ya Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka huduma za karibu zaidi na wananchi na kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro ina hospitali moja *DDH* na iko Loliondo kilometa zaidi ya 230; je, ni kinyume cha sera ya Wizara ya Afya kuwa na *DDH* mbili katika Wilaya moja?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya Wizara ya Afya mahali ambapo kuna *DDH* kwa kawaida tunasaidia *DDH* kuweza kutoa huduma. Lakini kama Wilaya yenyewe itaona kwamba kuna umuhimu wa kuwa Hospitali ya kwao wenyewe ya Serikali kwa kweli huwa haikatazwi ilimradi wenyewe wanazo fedha ambazo wanaweza kujenga. Kwa hiyo, kama mahitaji ni makubwa kunaweza kukawa na hospitali ya Serikali na wakati huo huo ikawa na Hospitali ya *DDH*. Kwa hiyo, sera haizuii.

Na. 11

**Kutungwa kwa Sheria ya Kudhibiti na Kuzuia Maambukizi ya UKIMWI**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Tume ya Kudhibiti UKIMWI, inakusanya maoni kwa ajili ya kutunga sheria ya Kudhibiti na Kuzuia Maambukizi ya UKIMWI.

(a) Je, ni maeneo gani ambayo wadau wanaona kuwa ni vyema yatungiwe sheria hiyo?

(b) Je, ni lini sheria hiyo italetwa Bungeni hasa ikizingatiwa kuwa taarifa mbalimbali zinazoonyesha kuwa karibu Watanzania milioni mbili wanaishi na virusi vya UKIMWI na maambukizi yanaendelea?

**NAIBU WAZIRI WA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Maeneo ambayo yataangaliwa na sheria inayopendekezwa ni kulenga jamii kwa ujumla kuhusu elimu kwa umma, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na watoa huduma ili wapewe tiba ya kinga iwapo watakuwa wamekumbana na maambukizi kwa bahati mbaya katika utendaji kazi wao *(Post Exposure Prophylaxis).* Aidha, Serikali itaangalia maeneo yafuatayo:-

(i) Kupunguza unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

(ii) Kutoa adhabu kwa wote watakaobainika kuambikiza virusi vya UKIMWI kwa makusudi.

(iii) Kuhakikisha damu inayotolewa kwa wagonjwa ni salama.

(iv) Kuhakikisha usalama wa watoa huduma za afya kuhusu maambukizi.

(v) Kuongeza kasi ya upimaji wa virusi vya UKIMWI katika vituo vya kutolea huduma.

(vi) Kutoa adhabu kwa mtu binafsi au taasisi kwa kupotosha jamii kuhusu masuala ya kinga pamoja na tiba ya UKIMWI.

Maeneo ambayo wadau wamependekeza hayana tofauti kubwa na ambayo Serikali imependekeza. Maeneo hayo ni kuongeza kasi ya kuelimisha umma kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI na misaada mbalimbali kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia masuala ya haki za binadamu katika upimaji wa virusi vya UKIMWI, unyanyapaa na utunzaji wa siri kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI, masuala ya haki na mali za wajane na yatima wa UKIMWI na haja ya kupima virusi vya UKIMWI kwa watoto wanaozaliwa.

Pia upimaji wa Virusi vya UKIMWI kabla ya kuanza shule na kabla ya kuingia katika ajira, upimaji wa virusi vya UKIMWI wageni wote wanaoingia nchini, kuwabana wanaofanya mapenzi na taahira na watoto wa mitaani, kuwapima virusi vya UKIMWI akina mama wajawazito na waume zao na bima ya afya kumgharamia aliyeambukizwa virusi vya UKIMWI kwa asilimia mia moja.

(b) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tayari imewasilisha Waraka kwenye Baraza la Mawaziri kuhusu pendekezo la kutunga sheria na Waraka huo umeshajadiliwa

na kupata baraka zake. Sasa hivi uko kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria na utakapokamilika utawasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2007.

Na. 12

**Hospitali yenye hadhi ya Mkoa – Dar es Salaam**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI (k.n.y. MHE. IDD M. AZZAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam hakuna hospitali yenye hadhi ya Mkoa, hivyo husababisha msongamano wa huduma katika Hospitali za Mwanyamala, Amana, Temeke na Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili;

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga hospitali yenye hadhi ya Mkoa katika Jiji ya Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaohitaji huduma katika hospitali nilizotaja?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Jiji la Dar es Salaam, hakuna hospitali yenye hadhi ya Hospitali ya Mkoa na hivyo kusababisha msongamano wa wagonjwa katika Hospitali za Manispaa za Amana, Temeke na Kinondoni na hata katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeliona tatizo hilo na inakusudia kulitatua. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ndiyo yenye jukumu la kujenga hospitali hiyo tayari imefanya makubaliano na shirika lisilo la Kiserikali la *CCBRT* ili kujenga hospitali yenye hadhi ya hospitali ya Mkoa katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mwaka ujao wa fedha zimetengwa shilingi 692,604,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi walioajiriwa na *CCBRT* na watakaoajiriwa kufanyakazi katika hospitali hiyo tarajiwa. *(Makofi)*

Aidha, iko mipango mingine ya ujenzi wa hospitali za kisasa katika Jiji la Dar es Salaam inayofanywa na Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya China na Shirika lisilo la Kiserikali la *TOKUSHUKAI Medical Corporation* la Japan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa mipango yote hii niliyotaja hapo juu utakapokamilika utasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaohitaji huduma katika Mkoa/Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la wagonjwa na matibabu ni suala la msingi katika sera yetu, katika Jimbo la Kilwa Kaskazini tunayo hospitali moja ya Misheni ambayo ilikuwa haina *x-ray* kabisa lakini tumejikakamua mpaka tumepata *x-ray* lakini Serikali inatoa tamko gani ili na sisi tujengewe *x-ray* tuliyoletewa ambayo tumeitafuta kwa udi na uvumba miaka kadhaa iliyopita na sasa hivi inaoza tu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa *x-ray* katika hospitali ya Kilwa Kipatimo ambayo ina *x-ray* ambayo haijapata, basi tutashauriana na Wizara yangu kuona ni jinsi gani tutawasaidia ili *x-ray* hii ambayo wameitafuta kwa udi na uvumba iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Na. 13

**Mkoa wa Morogoro Kuteuliwa kuwa na Ghala la Chakula**

**MHE. MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (k.n.y. DR. OMAR O. NIBUKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameuteua Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la Chakula, na kwa vyovyote vile ili kufanikisha mradi huo mkubwa unahitaji mkakati kabambe wenye gharama kubwa kiasi kwamba Mkoa peke yake hauwezi kumudu:-

(a) Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuusaidia Mkoa katika kufanikisha mradi huo muhimu sana kwa Taifa letu?

(b) Kama mkakati huo upo; je, Serikali imeshaandaa au kuagiza matrekta mangapi pamoja na pembejeo nyingine katika kufanikisha mradi huo?

(c) Je, mradi utagharimu fedha kiasi gani kwa kuanzia?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Mzeru Omar Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nia kubwa ya Rais katika kutangaza rasmi Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Chakula la Taifa ni kuhamasisha wananchi na viongozi wa Mkoa wa Morogoro na sisi wote katika ngazi ya Taifa kutumia mazingira ya rutuba iliyopo Mkoani Morogoro kwa jumla, kukuza kilimo na uzalishaji wa mazao ya chakula, ili Mkoa wa Morogoro uchangie kwa kiasi kikubwa katika kuondoa upungufu wa chakula unaojitokeza mara kwa mara kutokana na ukame. Kwa kuzingatia azma hiyo tarehe 24 Machi, 2007, ulifanyika mkutano Mkoani Morogoro na kuarifiwa kuundwa

timu ya wataalamu 20 waliopewa jukumu la kuandaa mpango maalumu wenye lengo la kutekeleza agizo hilo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeupokea mpango huo wa Mkoa wa Morogoro na tunaufanyia uchambuzi ili kubaini ni shughuli zipi zitatekelezwa katika ngazi ya Wilaya na Mkoa na zipi zitekelezwe katika ngazi ya Kitaifa, kwa kushirikisha sekta binafsi. Aidha, Wizara yangu inategemea kwa kiasi kikubwa kwamba Wilaya na Mkoa wa Morogoro, wataanza mara moja utekelezaji wa mpango huo kupitia programu ya Kuendeleza Kilimo Nchini *(Agricultural Sector Development Program - ASDP).* Programu ambayo inatoa fedha kila mwaka kuendeleza kilimo kupitia Halmashauri za Wilaya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama wote tunavyojua, jukumu la Serikali katika uchumi wa soko, ni kuweka mazingira ambayo yanavutia wawekezaji wa ndani na nje, kuwekeza na hivyo kuagiza na kufikisha zana za pembejeo mbalimbali kwa wakulima. Wizara yangu itashirikiana na uongozi wa Mkoa wa Morogoro, kuwashawishi na kuwatia moyo wawekezaji katika Sekta ya Kilimo kuelekeza mitaji yao katika Mkoa wa Morogoro ili washiriki katika utekelezaji wa mpango kabambe wa kilimo katika Mkoa wa Morogoro.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kilimo wa Mkoa wa Morogoro umekadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 105 katika kipindi cha miaka mitatu yaani kuanzia mwaka 2007/2008, kiasi ambacho ni kikubwa kupatikana kupitia Bajeti ya Serikali. Lakini kwa kushirikisha sekta binafsi, mpango huo utaweza kutekelezwa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa Serikali imekiri kwamba Mkoa wa Morogoro ni Ghala la Taifa na kwa kuwa vile vile mkoa huo huo uliwahi kuandaliwa mpango ambao wakati ule ulikuwa unaitwa Mpango wa Reli ya Uhuru. Sasa Waziri anaweza akatuambia wananchi wa mkoa ule na watalaamu mbalimbali watashirikishwaje katika utekelezaji wa mpango huo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mipango mingi ya kilimo imewahi kupangwa katika siku zilizopita baadhi ilitekelezwa kwa kiasi na mingine haikuweza kutekelezwa kabisa. Ni kweli vile vile kwamba Mkoa wa Morogoro unatambulika kwa mazingira kwa kuwa na rutuba na ardhi nzuri na vile vile na mvua za kutosha ukilinganisha na mikoa mingine nchini. Ni kutokana na msimamo huo ambao Mheshimiwa Rais, alitaka utengenezwe mpango ambao utafanya rutuba na mazingira ya Morogoro yaweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa chakula.

Kama tulivyosema katika jibu la msingi mpango umekwishatengenezwa unafanyiwa uchambuzi. Kwa kweli ni vigumu sana kusema ya kwamba Serikali inaweza ikatekeleza kwa sababu utekelezaji wa Mpango wa Kilimo utatekelezwa na wakulima ambao kwa kawaida ni watu binafsi. Tunachofanya katika Mkoa wa Morogoro kama tunavyofanya katika sehemu nyingine ya nchi ni kushirikisha wakulima kupitia programu ya uboreshaji wa kilimo ili kuhakikisha kwamba tunatumia fedha na rasilimali iliyopo,

kuongeza miradi ya umwagiliaji maji na kufikisha huduma ya maarifa kwa wakulima ili waongeze uzalishaji. Hivyo ndivyo tutakavyofanya.

Lakini katika Mkoa wa Morogoro tutafanya zaidi ya hapo kwa kushirikisha watu binafsi na kutoa motisha inayowezekana ili wakulima wa ndani na nje watumie rasilimali ya ardhi iliyoko katika Mkoa wa Morogoro kuongeza uzalishaji wa chakula. *(Makofi)*

Na. 14

**Mafao ya Wastaafu wa Jeshi la Wananchi**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao wamefariki bila kupata mafao:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotakiwa kufuatwa na warithi wa Marehemu ili waweze kupata mafao yao?

(b) Kwa kuwa kuna wastaafu waliochukua pensheni ya mkupuo na wamerejeshwa kwenye kitabu cha malipo na kujaza mkataba na *TRA* tangu Juni, 2004 lakini hadi leo hawajalipwa. Je, wastaafu hao wafanye nini ili waweze kulipwa malipo yao na Serikali inasema nini kuhusu wastaafu hao?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Jimbo la Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Jeshi za mwaka 1967 zinaelezea utaratibu unaotakiwa kufuatwa na warithi wa marehemu ili waweze kupata mafao yao. Utaratibu huo ni kama ufuatao:-

(1) Ndugu wa marehemu kukaa na kumteua msimamizi wa mirathi.

(2) Msimamizi wa mirathi atalazimika kufuatilia mahakamani taratibu za madai ya mirathi.

(3) Msimamizi wa mirathi atalazimika kuwa na nyaraka zifuatazo:-

(a) Barua ya mahakama alikowasilisha madai ya mirathi.

(b) Uamuzi wa mahakama juu ya mirathi.

(c) Fomu ya usimamizi wa mirathi.

(d) Kiapo cha kutunza watoto.

(e) Cheti cha ndoa.

(f) Vyeti vya kuzaliwa watoto chini ya miaka 21, na picha zao mbili mbili na zigongwe muhuri wa Mahakama nyuma na kusainiwa na Hakimu.

(g) Picha tatu za msimamizi wa mirathi na zigongwe muhuri wa Mahakama na saini ya Hakimu.

(h) *Pay Slip* ya mshahara wa mwisho wa Marehemu.

Baada ya kukamilisha nyaraka zote hizo, msimamizi wa mirathi ataziwasilisha katika kikosi cha marehemu au Makao Makuu ya Jeshi kwa ajili ya kukamilisha taratibu zilizosalia ambazo zitafanywa na Makao Makuu ya Jeshi na Hazina.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwarejesha kwenye daftari la pensheni wastaafu wote wa Serikali waliochukuwa pensheni zao kwa mkupuo, wakiwemo wanajeshi, lilifanywa kwa ukamilifu na kwa ufanisi zaidi na Wizara ya Fedha kupitia Hazina Ndogo za Mikoa. Wastaafu waliochukuwa pensheni kwa mkupuo walisajiliwa upya kwa kujaza mkataba na Hazina na sio *TRA* kama swali linavyoeleza.

Wastaafu waliotimiza miaka 10 tokea kuchukua pensheni zao kwa mkupuo, ndio waliokuwa na sifa za kuanza kulipwa pensheni kwa mujibu wa utaratibu mpya uliowekwa. Kwa wale ambao walichukua pensheni zao kwa mkupuo na hawajatimiza miaka 10 tokea wapatiwe malipo hayo, walipaswa kusubiri hadi muda huo utakapofikia ndio waanze kuingia katika utaratibu mpya wa malipo ya pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuwasaidia wastaafu na kama yupo mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye ana sifa na hapati haki zake, naomba awasiliane na Makao Makuu ya Jeshi, Idara ya Pensheni, ili aweze kusaidiwa na hatimaye kupata malipo yake. Aidha, Serikali itaendelea kuwasaidia wastaafu, kila itakapoona kuna haja ya kufanya hivyo kwa kuzingatia hali ya uchumi na kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la mafao kwa wastaafu kutoka Zanzibar wanapata usumbufu mkubwa sana kwa kufuatilia Dar es Salaam na bila ya mafanikio.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani ili kuweza kuondoa usumbufu huo?

(b) Je, Serikali haioni iko haja ya kuweka kitengo kule Zanzibar ili wastaafu wakafuatilie Zanzibar kuondokana na usumbufu huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu tunaotumia baada ya kukamilisha taratibu zote hundi zinakwenda katika Makao Makuu ya Jeshi, Kikosi cha Nyuki kilichopo Zanzibar. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, walikwishawahi kunifuata ofisini kuuliza hundi za watu wao waliopo katika majimbo yao. Kwa bahati nzuri nikawaelekeza na hundi zile wamezikuta pale pale Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu swali liliulizwa na Upinzani nitampa nafasi Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nina swali lifuatalo. Ameeleza kuwa wale ambao hawana miaka 10 inabidi wasubiri mpaka itimie miaka 10 ndiyo waingizwe kwenye utaratibu mpya. Lakini hali halisi ya maisha inamkwaza sana mtu ambaye ana dhiki.

Je, Wizara haioni wakati umefika sasa wa kutazama upya utaratibu huo ili kuweza kuwasaidia wale wastaafu wasiendelee kuteseka katika maisha haya magumu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ifahamike kuwa wastaafu hawa walilipwa kwa mkupuo.

Narudia, wastaafu hawa walilipwa kwa mkupuo, awali sheria ilikuwa inatoa miaka kumi na mbili na nusu, baadaye ikafanyiwa marekebisho ikaenda mpaka miaka kumi na tano na nusu. Hawa walikwishachukua haki zao kwa mkupuo, walilazimika kusubiri mpaka miaka kumi na mbili na nusu itimie ndiyo warejeshwe tena kulipwa.

Lakini Serikali ilichofanya imesema kwamba kama wameshatimiza miaka 10 toka wamechukua haki zao, hawa wameshamalizana na Serikali. Lakini Serikali imewarudisha tena kwa imani ya Serikali, kama mtu kapewa miaka 16, Serikali ikamwambia baada ya miaka 10 unarudishwa. Mimi nadhani kwa kweli tuipongeze sana Serikali. *(Makofi)*

Na. 15

**Vijana Waliojiunga na JKT**

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kujibu hoja za Wabunge waliochangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tarehe 3 Julai, 2006 Serikali kupitia Wizara hiyo ilitamka kwamba, kutakuwa na ongezeko la vijana kutoka Zanzibar watakaojiunga na JKT:-

(a) Je, ni vijana wangapi kutoka Tanzania - Zanzibar hadi sasa wamejiunga na JKT?

(b) Je, ni vigezo gani vilivyozingatiwa katika kuwapata vijana hao?

(c) Je, kati ya vijana hao, ni wangapi wa kike na wangapi wa kiume?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mnamo tarehe 3 Julai, 2006 alieleza kwamba, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itaongeza idadi ya vijana wanaojiunga na JKT kila pale nafasi itakapokuwa inapatikana. Lengo la Serikali ni kuona kwamba vijana wengi wanapatiwa mafunzo ya ulinzi na ukakamavu.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya vijana 370 kutoka Tanzania - Zanzibar wamejiunga na JKT hadi sasa tokea shughuli za JKT zirejeshwe mwaka 2001. Aidha, vijana 260 kutoka Zanzibar wanatarajiwa kujiunga na kambi mbalimbali za JKT wiki hii katika Operesheni ya Maisha Bora.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivyotumika katika kuwapata vijana hao ni kwanza uraia, awe ni Mtanzania, amemaliza darasa la saba na kuendelea, awe na umri si chini ya miaka 18, awe na afya, mwaadilifu (asiwe mhalifu) na awe amepitishwa na Serikali za Mitaa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijana hao 370, vijana wa kiume 336 na vijana wa kike ni 34.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona na mimi naomba niulize swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania ni moja na kwa kuwa kule Zanzibar nako kuna jeshi kama hili, ingawa haliitwi JKT lakini linaitwa JKU; je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba hakuna haja ya kuwa na majeshi mawili nchi moja na hivyo kuna umuhimu sasa wa kulifuta mara moja JKU? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo tulikwishaulizwa tukajibu. JKT limetungwa kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bunge hili na JKU imetungwa na sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi siyo vyombo vya Muungano. Lakini JKT ina sura ya Kitaifa, tukasema kama suala la kufutwa JKU, Baraza la Wawakilishi ndiyo

wafanye maamuzi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kulifuta JKU na siyo Bunge hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naona nilitaka kupendelea *gender*, sasa naona Mkuu wa Upinzani amesimama.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba JKT siyo jeshi la Muungano. Anaweza kusahihisha usemi wake? Kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya nchi Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni jeshi la Muungano wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndiyo jeshi kwa mujibu wa Sheria kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ndiyo jeshi la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa siyo jeshi la Muungano na nataka niseme hivyo kwa sababu wakati fulani Wazanzibar wenyewe walitaka JKT liondolewe katika Wizara ya Muungano. Kwa hivyo, mimi nathibitisha kwamba JKT siyo Jeshi la Muungano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali katika Wizara ya Usalama wa Raia. Akishaitwa kiongozi wako basi tunaendelea. *(Kicheko)*

Na. 16

**Ujambazi wa Kutumia Silaha**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa vitendo vya kutisha vya ujambazi wa kutumia silaha vimetokea kwa miaka mitatu mfululizo tangu mwaka 2004 na vimesababisha vifo vya watu hususan kwenye eneo liitwalo Daraja Mbili kwenye barabara inayotoka Mikumi kwenda kwenye viwanda viwili vya sukari vya Kilombero katika kijiji cha Ruaha:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kukipatia kituo cha Polisi Mikumi gari moja zaidi lililo imara hasa ukitilia maanani kuwa kituo hicho kina gari chakavu na kituo cha polisi Ruhembe kilichopo kiwandani hakijawahi kupewa gari kwa zaidi ya miaka 25 ili kwa pamoja vikipatiwa gari viweze kukabiliana na wimbi la ujambazi ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi la polisi linakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi yakiwemo magari yenye kukidhi mahitaji kwa mikoa yote ya Tanzania. Kutokana na ufinyu wa Bajeti na uwezo mdogo wa Serikali, bado zipo Wilaya chache ambazo hazijapatiwa magari mapya. Hata hivyo, Serikali itafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba Wilaya hizo zinapata magari, ikiwa ni pamoja na kituo cha Mikumi. Kwa hali ya fedha ilivyo sasa tutaendelea kulifanyia matengenezo gari lililopo Mikumi ili liweze kutoa huduma ya kuridhisha.

Aidha, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya polisi kikiwemo kituo kidogo cha Ruhembe vinapata vyombo vya usafiri yakiwemo magari na pikipiki hatua kwa hatua kadri ya hali ya fedha ya Serikali itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi la polisi linaendelea kufanya doria, misako na utekelezaji wa dhana ya ulinzi shirikishi *(community policy)* na ulinzi jirani *(neighbourhood watch)* ili kukabiliana na uhalifu katika mji wa Mikumi na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru wananchi wote ambao wanashirikiana na jeshi la polisi katika kupambana na uhalifu ili tuweze kuutokomeza wote kwa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Nimshukuru Naibu Waziri kwa kupata fursa ya kuja kututembelea katika eneo la matukio ambayo yanajirudia rudia katika eneo la ukanda wa pale Mikumi katika Daraja Mbili.

Kwa kuwa tangu alipotembelea tarehe 28 Machi, 2007 matukio ya ujambazi wa kutumia silaha yameendelea na yametokea matukio matatu, mawili yakihusisha wizi na ujambazi katika hoteli za utalii na moja tarehe 23 Mei, 2007 lililohusisha majambazi kutega mawe na mimi pamoja na baadhi ya wananchi tuliokuwa njiani kunusurika kuvamiwa na majambazi; je, Serikali haioni kuwa eneo hilo ambalo lipo jirani kabisa na Kambi ya Jeshi la Wananchi Mikumi, lichukuliwe hatua za haraka na za kudumu, kwa kuweka geti au kutoa gari ya dharura ili kufanya doria za mara kwa mara kupambana na ujambazi huo?

Pili, niwie radhi Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa eneo lile halina mawasiliano, lina mtandao wa kilomita saba hivi. Upande ule wa Magharibi wa barabara hii ya kilomita saba eneo hilo linamilikiwa au liko chini ya himaya ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania;

Je, Serikali haioni kwamba ungepatikana ufumbuzi wa kudumu wa haraka kusudi kuondoa hisia zozote zisizokuwa sahihi za kuweza kuwapaka madoa wananchi au wanajeshi wetu shupavu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuhusiana na tukio hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Beatus Lyamba kwa ushirikiano mkubwa alionao na Wizara yetu na kushirikiana na sisi wakati wa ziara ile kufika pale Daraja Mbili. Hii inaonyesha wazi imani yake juu ya wananchi wa Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumetokea matukio katika eneo la Daraja Mbili na hivi sasa Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha doria na misako na kushirikiana na wenzetu wa JWTZ ili kupata ufumbuzi wa kudumu katika eneo lile. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya kila jitihada kuhakikisha wananchi wa eneo lile wanakuwa salama na maeneo yote katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mazungumzo yanaendelea kati yetu na JWTZ kuhakikisha kwamba ufumbuzi wa pale unapatikana ili kuepuka madhara mengine yasitokee huko mbele na kuondoa dhana ya kufikiriwa vibaya wanajeshi wetu wa JWTZ. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutachukua hatua za ziada ili hali iwe nzuri katika eneo lile. *(Makofi)*

Na. 17

**Mahitaji ya Kiwanda cha Saruji – Itigi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Tarafa ya Itigi kuna hazina kubwa ya madini ya *gypsum* au jasi na kwa kuwa kuna miundombinu ya reli ya kati na barabara zinazounganisha pande zote za nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashawishi wawekezaji kujenga kiwanda cha saruji Itigi ili saruji iweze kusambazwa kwa gharama nafuu zaidi Mikoa ya Kati na Magharibi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa saruji hiyo ikizalishwa kwa wingi itapata soko la uhakika nchi jirani za Maziwa Makuu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa Tarafa ya Itigi inayo hazina ya madini aina ya *gypsum* au jasi ambayo ni moja ya malighafi inayotumika katika kutengeneza saruji. Lakini pia naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa madini ya jasi siyo malighafi pekee inayotumika kutengenezea saruji. Madini ya jasi huchukua takriban asilimia tano tu ya mahitaji yote

ya malighafi inayotumika kutengenezea saruji. Malighafi nyingine muhimu ambayo Serikali kwa sasa bado haina taarifa iwapo nayo inapatikana huko Itigi ni madini aina ya chokaa *(limestone)* ambayo matumizi yake ni takriban asilimia sabini na tano pamoja na udongo mwekundu *(redsoil)* ambayo matumizi yake ni kama asilimia ishirini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miundombinu ya reli ya kati na barabara zinazoiunganisha Itigi na pande zote za nchi kuiwezesha kuwa na kiwanda cha saruji, uhamasishaji wa kujenga kiwanda hicho hauwezi kufanyika kwa sasa mpaka taarifa za upatikanaji wa malighafi nyingine nilizozitaja zitakapopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jasi inayopatikana huko Itigi inao ubora unaofaa kwa matumizi ya kutengenezea bidhaa nyingine kama chaki na *Plaster of Paris (POP),* Serikali kwa sasa inatoa wito kwa wawekezaji watakaoweza kutumia jasi hiyo kutengenezea bidhaa hizo. Aidha, Serikali itavishauri viwanda vya saruji vilivyo nchini kuangalia uwezekano wa kununua jasi kutoka Itigi kwa ajili ya matumizi ya kutengenezea saruji kwenye viwanda hivyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:**Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana kusikia kwamba Serikali haina uhakika juu ya kuweko kwa chokaa Itigi. Miaka mingi chokaa imekuwa ikizalishwa Itigi na imesafirishwa katika viwanda mbalimbali vya saruji kule Tanga pamoja na Mbeya na hata huu udongo mwekundu upo. Hivi vyote jasi, chokaa na udongo mwekundu vipo. Halafu tuna umeme, sasa vitu hivi vinazalishwa, vinarudishwa nyuma wanasafirisha mpaka Tanga saruji izalishwe kule halafu ndiyo tupatiwe saruji mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vitu vyote hivi vipo; na kwa kuwa hajanipa *time frame* wala kufikiria kwamba wana mkakati upi wa kuweza kuwashawishi wawekezaji, ningeomba Waziri mhusika anipe jibu la uhakika ni lini Serikali hasa itafikiria kuweka kiwanda Itigi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, jibu la nyongeza je, hufahamu kweli? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jibu langu sijasema kwamba sifahamu chokaa haipo Itigi. Nilichokisema ni kwamba kwa sababu swali la msingi liliuliza madini aina ya jasi ambayo yanapatikana kwa wingi inasababisha kuweka kiwanda cha saruji. Nilichosema ni kwamba kwa sababu hatujapata taarifa za ukamilifu wa hizi malighafi nyingine, bado hatuwezi tukahamasisha uwekezaji? Lakini kwa uhakika nilichokieleza katika jibu hapa ni kwamba endapo taarifa hizo zitakuwa zimepatikana kwa ukamilifu, kwa vyovyote vile tunatoa wito kwa wawekezaji wakawekeze ujenzi wa kiwanda kule Itigi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala la kuweka *time frame* hatuwezi kuweka *time frame* kwa sababu swali lenyewe linasema kwamba tuhamasishe. Mimi nataka nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wawekezaji wote ambao wana nia ya kuwekeza katika kujenga kiwanda kule Itigi

waweze kufanya hivyo ilimradi malighafi hizi nilizozitaja zinapatikana kwa wingi unaostahili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kupitia Bunge hili wawekezaji wamesikia. Nataka kumaliza maswali yote.

Na. 18

**Uchakavu wa Reli na Treni**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa abiria na mizigo katika mkoa wa Kigoma ni wa kutumia reli; na kwa kuwa reli na treni zinaonekana kuchoka hali inayosababisha ajali za mara kwa mara ambapo vifo na upotevu wa mali za watu hutokea:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu uchakavu wa reli hiyo na treni ili kunusuru maisha ya watu na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha njia ya Reli ya Kati upo mpango wa muda mrefu wa kupanua geji ya reli kufikia reli yenye upana wa *1435mm (standard gauge)* na uzito wa reli wa ratili 120 kwa yadi. Mpango huu utafanikiwa pale tutakapopata fedha.

Kwa sasa tutaimarisha njia ya reli na kubadilisha mataruma yake kwa kutumia mkopo toka Benki ya Dunia ambao ulitolewa kwa mradi huu muda mrefu kidogo. Katika mradi huu reli za uzito wa paundi 80 kwa yadi pamoja na mataruma na vishikizo vyake zilishaagizwa na vimewasili tayari. Hivyo vitatumika kutandika kilomita 47 za njia ya Reli ya Kati ya Itigi na Tabora. Utandikaji utatarajiwa kuanza mwezi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo makubaliano na mwekezaji kuwa akarabati sehemu ya reli yenye urefu wa kilomita 648 katika kipindi chake cha ukodishaji, lakini makubaliano hayo ni ya kutumia *80lbs* reli, ili tuweze kufikia uzito wa *120lbs*/yadi. Serikali italazimika kufidia tofauti hiyo, pamoja na ile ya makubaliano ya awali ya mkopo wa Benki ya Dunia.

Katika kufanikisha azma yetu ya kuimarisha reli yetu kuwa ya uzito wa ratili 120 kwa yadi, tutahitajika pia kujenga kiwanda cha kutengeneza *congrete sleepers* hapa hapa nchini. Hivyo mradi huu kabambe utatekelezwa baada ya upatikanaji wa fedha na

tunategemea mradi utakapotekelezwa reli za uzito wa *801bs*/yadi zitahamishwa katika njia zetu fupi za Kaliua - Mpanda, Manyoni - Singida na Kilosa - Kidatu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Ahsante Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza yenye sehemu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa abiria wengi wanaosafiri na treni hutumia mabasi kutoka Dar es Salaam mpaka hapa Dodoma na mara nyingi mabasi mengine huchelewa kufika na kusababisha abiria kukuta treni imeondokana kuwasababishia wasafiri kupata shida wanapokuwa wameachwa na treni; je, Serikali wakati inaendelea na maandalizi hayo ina mpango gani wa makusudi wa kuweza kuwasaidia abiria wanaokuwa wameachwa na treni na hasa wanawake na watoto? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa bandari ya Kigoma ni lango kuu la biashara katika uchumi kwa nchi ya Jamhuri ya Kongo na Burundi; je, Serikali itakubali kuelimishwa kuhusu barabara za lami barabara ya Kigoma, Malagarasi, Tabora - Manyoni, Tunduma - Sumbawanga hadi Kigoma na ile barabara ya kutoka Kigoma – Kasulu - Kibondo hadi Nyakanazi kuwa ni muhimu kwa ajili ya kufungua uchumi wa nchi jirani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waachane na reli. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa na usafiri salama na wa wakati. Endapo kutatokea lolote lile ambalo linafanya wasafiri kupata shida barabarani kwa sababu ya ubovu wa magari, *TRC* inatoa kipaumbele hasa kwa wale ambao wanakwama.

Si rahisi kusema mtu amefika hapa saa 10 za jioni na treni imeshaondoka saa 9 za mchana tukasema tutatengeneza treni nyingine ya kumpeleka. Lakini tunahakikisha treni inayofuata wale wote ambao wamekwama wanapata usafiri na tutawaomba wenye mabasi wahakikishe mabasi yao ni salama yafike hapa mapema ili abiria wao waunganishe. Lakini pia tutawaomba abiria na wao wajue kwamba wanasafiri saa fulani watoe muda wa kutosha wafike Dodoma ili kuwahi treni hiyo inayokwenda.

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Kigoma ni bandari ambayo inaunganisha lango kuu la usafiri kwa *DRC Congo,* Rwanda na Burundi na ndiyo maana tumeweka hatua za makusudi kabisa kutengeneza hizi barabara Mheshimiwa Mbunge alizozisema. *(Makofi)*

Na. 19

**Usafirishaji kwa Njia ya Bandari**

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu bado ina matatizo makubwa ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya bahari kutoka Dar es Salaam – Zanzibar – Dar es Salaam, na kwa kuwa vyombo hivyo vinapopata ajali husababisha vifo vya watu na bidhaa nyingi kupotea:-

(a) Je, Serikali inavitambua vyombo hivyo?

(b) Je, Serikali inafanya ukaguzi wa kutambua kwamba kila mwenye chombo amekata bima?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdulraaman Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inavitambua vyombo vya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya bahari na imevisajili kwa ajili ya kutoa huduma zinazotolewa. Aidha, hali ya usafirishaji wa mizigo kati ya Dar es Salaam – Zanzibar - Dar es Salaam kwa sasa imeimarika kwa kiwango kikubwa hasa ikizingatiwa kuwa mizigo mingi husafirishwa kwa meli.

Kwa mfano, meli zifuatazo na uwezo wake wa kubeba mizigo hufanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Zanzibar, *MV Aziza 1* (tani 350), *MV Aziza 2* (tani 400), *MV Mudahiri* (tani 250), *MV Maendeleo* (tani 650). Aidha, kuanzia mwaka 2006 huduma za meli za kubeba mizigo ndani ya makasha *(containerized cargo)* kati ya miji ya Dar es Salaam – Zanzibar - Tanga zimekuwa zikitolewa na meli za *MV Royal Zanzibar* (tani 1700 au makasha 61) na *MV Mantehna* (tani 1600 au makasha 94). *(Makofi)*

Hata hivyo, sambamba na vyombo hivi yapo majahazi yenye uwezo tofauti yanayobeba mizigo mbalimbali kati ya bandari hizi. Kwa msingi huo hakuna dalili za mrundikano wa mizigo inayotakiwa kusafirishwa kati ya miji hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu kubwa ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya bahari kati ya Dar es Salaam na Zanzibar inafanywa na vyombo vilivyokaguliwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. Ili kuimarisha usalama na ufanisi wa sekta ya usafiri wa majini Serikali zote mbili kwa pamoja huweka mikakati ya kuwezesha viwango na matakwa ya usafishaji na kuwa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukaguzi wa kila mwaka *(annual surveys),* ukaguzi mwingine huweza kufanywa kwa chombo chochote wakati wowote ule ili kuhakiki ubora wake na kuhakikisha kuwa hakipakii zaidi ya uwezo wake. Pale inapobainika kuwa chombo hicho kinaendesha shughuli zake bila kuwa kimekaguliwa na kupewa cheti cha ubora au kina upungufu, hatua za haraka huchukuliwa kukikagua na ikibidi kukisimamisha kutoa huduma hadi kitakapokaguliwa tena na kudhihirika kuwa kina ubora unaostahili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003, Sehemu ya III, Kifungu cha 11 kinatamka kuwa chombo chochote chenye uwezo wa kubeba

abiria au mizigo ni lazima kiwe na bima kwa ajili ya kulipa fidia kwa watu wengine wanaoweza kupata hasara kwenye chombo hicho *(third party insurance cover).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* inasimamia ili kuhakikisha kuwa sheria hiyo inatekelezwa na vyombo vinakuwa na bima. Kwa sasa meli ya abiria au mizigo haipewi usajili au cheti cha ubora na *SUMATRA* bila kwanza kuwa na bima inayohitajika kisheria. Utaratibu huu unatarajiwa pia kuanza kutumika kwa vyombo kama majahazi yanayobeba abiria au mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iko katika hatua za kutengeneza kanuni zitakazotawala na kuboresha utendaji katika usafiri wa majini hususan kinga juu ya hasara kwa abiria na uchafuzi wa mazingira. Kanuni hizi zinatoa maelekezo ya wazi zaidi juu ya bima ukiwemo utekelezaji wa bima kwa vyombo vidogo kama majahazi. *(Makofi)*

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa nini Serikali inaviachia vyombo hivi vya majahazi kuweza kuchukua abiria na mali zao bila ya bima na kuhatarisha maisha ya wananchi na mali za wananchi, kwa mfano *MV Takrima* iliyozama Msasani wakati inaondoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba Sheria ya Usafiri Majini ambayo *SUMATRA* imeisimamia inasema wazi kabisa si ruhusa kwa meli kutembea bila kuwa na bima na hiyo ndiyo inayokaziwa, kama *MV Takrima* ilifanya hivyo ilifanya makosa. *(Makofi)*

Na. 20

**Mawasiliano ya Barabara**

**MHE. TATU M. NTIMIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya kukatika kwa mawasiliano ya barabara kati ya Kijiji na Kijiji, Kata hadi Kata, Wilaya hadi Wilaya na Mkoa hadi Mkoa; na kwa kuwa, Serikali ilitoa shilingi bilioni 10 ili angalau kurudisha mawasiliano hayo nchi nzima:-

(a) Je, fedha hizo zimepelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ngapi hadi leo?

(b) Je, Wilaya ya Uyui imepelekewa lini fedha hizo na ni kiasi gani kimepelekwa?

(c) Kwa kuwa Serikali kupitia Waziri wa Miundombinu ilipokuwa ikitoa majibu ya nyongeza kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa George Lubeleje katika Mkutano wa Saba ilieleza kuwa fedha hizo za dharura zilitolewa kwa lengo la kurudisha mawasiliano ya barabara kati ya Mkoa na Mkoa;

Je, Serikali inaweza kunihakikishia kuwa, ni kiasi gani cha fedha kilitolewa kwa ajili hiyo kati ya Mkoa wa Tabora na Singida kwa kupitia barabara ya Itigi ambayo ni ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mvua zilizonyesha nchi nzima kati ya mwezi Oktoba, 2006 na mwezi Januari, 2007, uharibifu mkubwa wa barabara na madaraja ulitokea. Tathmini ya kwanza ya uharibifu huo iliyofanywa na *TANROADS* kwa barabara za Kitaifa yaani barabara kuu na barabara za Mkoa na kuwasilishwa Wizarani mwezi Januari, 2007 ilionyesha mahitaji ya fedha za dharura ya kiasi cha shilingi 10,364,833,000/= kwa nchi nzima. Lakini ni wazi kuwa baada ya hapo uharibifu umeendelea kuongezeka. Ili kupata fedha hizi za dharura kutoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu ilitakiwa kuwasilisha hati za madai ya Makandarasi kutoka Mikoani zinazoonyesha kuwa kazi za matengenezo zimefanyika kurekebisha uharibifu uliotokea. Wizara yangu imepokea hati hizo kwa awamu kutoka *TANROADS* na imeziwasilisha Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 10.4 zilizoombwa na Wizara ya Miundombinu zilikuwa ni kwa ajili ya barabara kuu na barabara za Mkoa zinazohudumiwa na *TANROADS*. Hivyo hakuna fedha kutoka katika fungu hilo la dharura zilizopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya.

(b) Wilaya ya Uyui kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya kama zilivyo Wilaya nyingine haijapelekewa fedha za dharura kutoka katika fungu hili la dharura.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na makadirio ya mwanzo, Mkoa wa Tabora uliomba jumla ya shilingi milioni 470.42 kwa ajili ya matengenezo ya dharura. Fedha hizi zimetolewa na Wizara ya Fedha katikati ya mwezi Mei, 2007 na kati ya fedha hizo barabara ya kutoka Tabora- Kigwe hadi mpakani mwa Singida imetengewa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kazi za dharura. Hali ya barabara hii kwa upande wa Mkoa wa Singida ni ya kuridhisha hivyo haikuombewa fedha za dharura.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kuunganisha Mkoa na Mkoa. Lakini Mkoa bila watu hauwezi kuwa Mkoa. Kuna Wilaya ambazo zilikuwa zimepata mafuriko sana, wananchi wakashindwa kutoka katika maeneo yao.

Je, isingekuwa muhimu kwamba Wilaya ambazo zilikuwa na mafuriko kiasi hicho zingetumika helikopta kuwapelekea chakula na dawa? Isingekuwa busara kwa Serikali kuweza kuunganisha Wilaya hizo na Mikoa yake ili wananchi waweze kupata huduma za muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na Wilaya ambazo zilipata athari kubwa sana za mvua na zilifungika, lakini Serikali kwa kutumia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa ilishughulikia matatizo haya Kitaifa. Lakini kuhusu kutenga fedha za barabara kwenye Wilaya hizo, kitu ambacho kilifanyika kwa wakati ule Wizara ya Miundombinu kupitia *TANROADS* iliomba fedha kwa ajili ya barabara ambazo zinahudumiwa na *TANROADS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo, ilitakiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kuangalia barabara ambazo zinashughulikiwa na Halmashauri mbalimbali iangalie namna gani ichukue hatua za dharura za kurekebisha hali ambayo ilikuwa imeharibiwa vibaya na mvua. Nadhani kwamba hilo lilifanyika na ndiyo maana kumeendelea kuwepo na mawasiliano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Tunapenda kwa makusudi kabisa wakati wa kipindi hiki cha Maswali na Majibu cha saa moja wale waliouliza maswali waweze kufikiwa. Maana haitakuwa na maana tunaacha maswali matatu kwa sababu ya maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, ndiyo maana nimejitahidi yamekwisha, kwa hiyo nimefurahi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu matangazo. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anawaomba Wajumbe wake wa Kamati ya Huduma za Jamii kuwa leo tarehe 13 Juni, 2007 saa 4.15 asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati kwenye chumba cha mikutano namba 231, ghorofa ya pili jengo la utawala.

Halafu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto anapenda kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote katika uzinduzi wa siku ya Mtoto wa Afrika ambao utafanyika leo hii mara baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu. Uzinduzi huo utafanyika katika Uwanja wa Jamhuri.

Aidha, kutakuwa na maonyesho mbalimbali yanayohusu Ustawi wa Watoto yatakayokuwa yanaendelea katika uwanja huo kwa wiki nzima na sikukuu ya Mtoto wa Afrika ni tarehe ya 16 Juni, 2007 siku ya Ijumaa.

Kwa hiyo, mnakaribishwa wote na hususan Kamati ya Maendeleo ya Jamii, lakini Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu, pale *Jamhuri* S*tadium.*

Halafu Mheshimiwa Zaynab Vulu, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika Mikoa inayolima zao la Korosho kwamba kutakuwa na kikao kati ya Wajumbe hao na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kikao hicho kitafanyika katika chumba namba 432 saa hakutaja, ghorofa ya nne. Saa ngapi?

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeandika kwenye karatasi yangu mara baada ya kuahirisha kikao hiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tangazo la mwisho la kazi. Kamati ya Utendaji ya Chama cha Wabunge Wanawake *(TWPG)* naomba tukutane baada ya kuahirisha kikao hiki kwenye Ofisi ya *TWPG. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu wageni waliopo mbele yetu, hapa leo tuna wageni wanafunzi na walimu 54 kutoka shule ya sekondari ya *The South Highlands* iliyoko Mafinga Iringa, wasimame wote. Karibuni, ahsante sana! *(Makofi)*

Halafu tuna wageni wanaotoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Jiji la Arusha. Naomba wasimame wote. Ahsante, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu leo ni tarehe 13 Juni, 2007 kazi yetu tunaishia kipindi cha Maswali na Majibu. Kesho asubuhi tutaanza na kipindi cha Maswali na Majibu. Halafu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji atasoma hotuba yake kisha tutaahirisha Bunge. Saa 10.00 jioni Waziri wa Fedha atasoma hotuba yake.

Kwa hiyo, wote muwahi kwa sababu tutakuwa na wageni kutoka sehemu mbalimbali za nchi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika!

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anajibu swali Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ametamka jambo ambalo kidogo limeleta hisia ambazo wengi tulikuwa hatufahamu kwamba JKT siyo Jeshi la Muungano na hii wengi wetu tulifikiri ni Jeshi la Muungano kufuatana na Ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatoa tafsiri; "kwa madhumuni ya Ibara hii mwanajeshi maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa."

Sasa hali hii inatupa wasiwasi nchi nzima na ndiyo maana wengine tulielewa alipojibu kwamba vijana mia tatu na kadhaa wameingia JKT tukajua wameenda mahali pao. Sasa kama Wazanzibari hawatambui JKT kuwa ni Jeshi la Muungano wameenda kule kufanya kitu gani?

Kwa hiyo, tungependa kupata ufafanuzi kwa sababu hili ni jambo ambalo ni la Kitaifa na watu wote waliomsikia Naibu Waziri natumaini na wenyewe wana mashaka kama vile mimi nilivyopata mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesimama, kama anataka naweza kutoa Mwongozo baadaye kama lazima.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa John Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mimi ninakubaliana kabisa na jibu alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu zifuatazo, Ibara aliyosema ni Ibara 147 ambayo pamoja na watu waliotajwa kwenye hiyo Ibara aliyosoma ni Jeshi la Magereza. Je, Jeshi la Magereza ni Jeshi la Muungano? Jeshi la Magereza lipo Tanzania Bara tu na limeanzishwa kwa sheria. Pia JKT ni Jeshi ambalo limeanzishwa kwa sheria na ile sheria siyo ya Muungano. Je, ni kambi ngapi za JKT ambazo ziko Zanzibar? Kama lingekuwa ni Jeshi la Muungano wangeanzisha kambi zao kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba JKT siyo Jeshi la Muungano. Wazanzibari wanaoingia JKT ni Watanzania na wanaingia kwenye Jeshi kama Watanzania. Wengi wa Wazanzibari wanakaa Tanzania Bara na wamesoma hapa Bara. Nadhani hayo niliyoyazungumza yanatosha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo gani? Siyo lile lile lililoulizwa!Kama ni jambo lile lile lililokwishajibiwa hatuwezi kuendelea na mjadala sasa. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 4.12 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 14 Juni, 2007 saa tatu asubuhi*)